# IMANI BILA MATENDO IMEKUFA. MAANDIKO: YAK. 1:22 – 25, Yak. 2: 14 – 26

1. **UTANGULIZI**
   Mojawapo ya silaha kabambe sana ambayo shetani amekuwa akiitumia mno kuchelewesha Baraka za watoto wa Mungu walizoahidiwa na Mungu wao ni kuwatisha ili wasichukue hatua juu za imani ya jambo Fulani ambalo Mungu ameahidi kuwapatia. Ndiyo sababu Mtume Yakobo anawaonya watu wote waliookoka kwamba kuwa na imani juu ya Yesu halafu ukawa siyo mtendaji wa kile ambacho umekiamini**, imani hiyo ni imani marehemu!!! Sote tunafahamu maana ya kufa kimwili maana yake ni kwamba roho na nafsi vinatengana na mwili, na mwili unabaki kuwa hauna thamani tena.**

- Mteule mwoga wa kuchukua hatua za imani bali akabakia kuwa fundi wa kusimulia tu mdomoni Ukuu wa Yesu Kristo kwa watu wengine kamwe asahau kuziona Baraka za Mungu wala kumwona Yesu akijidhihirisha kwake wakati wowote. Wataalamu wa mambo ya kiroho wanasema kwamba hatua moja tu ya imani anayoichukua mteule ya kulitenda neno la Mungu alilosikia/alilofundishwa na akalielewa inakuwa na thamani kubwa sana mbele za Mungu, na wakati wote hatua hiyo moja itasababisha matokeo makubwa sana katika maisha yake kuliko kuwa na malengo/mipango/au makusudi 1000 ambayo hayana hatua za utendaji. ***Math. 11:12.*** Lazima uchukue hatua za imani kwa kkitu/jambo ambalo umeliamini ili baadaye ndipo liwe dhahiri machoni pako. ***Ebr 11:1-6, Mark 11:22-24.***

- **Leo nirudie msemo niliwahi kuwaambia huko nyuma kwamba haijawahi kutokea popote duniani, na wala haitakaa itokee kamwe kwamba mtu amejikwaa mguu**

**wake kwenye kitu chochote akiwa amekaa chini!! Kukaa chini bila kuchukua hatua na bado utegemee Baraka, utegemee ushindi, utegemee kuponywa magonjwa yako, utegemee kuwa mtu mkubwa na aliyefanikiwa, utegemee kuyashuhudia matendo makuu ya Mungu katika maisha yako zitabakia kuwa hadithi na ndoto tu katika maisha yako yote. Chungu ni wadudu ambao hawasemi daima, bali wamejaa kuchukua hatua katika maisha yao yote, na ndiyo sababu wana chakula tele maisha yao yote na akiba tele wanayo na wanajenga vichuguu vikubwa ajabu - Mithali 6: 6 – 8.** Ndiyo sababu Yesu Kristo alimsifia sana tena sana Yohana Mbatizaji, yeye hakuogopa mtu yeyote katika utumishi waken alikuwa ni mtu wa kuchukua daima. ***Luk 3:1-14.***

2. Katika Biblia watu mashuhuri tunaosoma habari zao na kusisimuka; majibu ya maombi yao yalitokea wakati walipo chukua hatua ya imani ya kutenda kile ambacho Neno la Mungu limesema nao. ***Mfano:-***
   a. Ibrahimu – ***Mwnz. 12: 1 – 5, 22: 1 – 18***
   b. Rahabu – ***Yosh. 2: 1 – 24, 6: 21 – 23***.
   c. Ruth- Ruth. ***1: 15 – 18, 3: 1 – 18, 4: 13 – 22***
   d. Esta- ***Esta 4: 15 – 17, 5: 1 – 4, 7: 1-10, 8:15 – 17, 9: 17 – 19***
   e. Mark***. 5: 25 - 34.***
   f. Bartholomayo kipofu – ***Mark. 10: 46 – 52***
   g. Hana – ***1Samwl. 1: 10 – 20***
   h. Wakoma wanne – ***2Wafal. 7: 3 – 11***
   i. Daudi - ***1Samwl. 17: 41 - 54, 1Samwl. 18: 6 - 9*** n.k.

   - Hii ndiyo sababu kubwa ya mama yake na Yesu (Mariamu) kuwaambia mapema kabisa wanafunzi wa Yesu kwamba lolote
   atakalowaambia, ninyi fanyeni (mlitende) –***Yoh. 2: 3 – 11.***

3. **Ngoja niwafundishe jambo hili muhimu kwamba kamwe kamwe shetani hamwogopi mteule anayekiri mdomoni sana kwamba ameokoka, maana kama ni kukiri yeye ni**

**fundi mno tena anakiri kwa kutetemeka kabisa.** Yako. 2: **19 – Bali shetani anamwogopa mno mteule ambaye ana tabia ya kulitenda Neno la Mungu analofundishwa. (yaani wapendwa, majibu ya maombi yetu wakati wote** yataambatana/yatatokana na hatua zetu za imani tunazochukua baada ya kuomba) ***Yak. 1: 22, 2: 26.***

- **Mungu kamwe hapendezwi na mteule aliyejaa na simulizi za neno lake kama historia tu, bali daima anapendezwa na mteule anayechukua hatua za imani za kulitenda Neno lake Takatifu katika maisha yake.** ***Ezek. 33: 30 – 33.***
- **Ngoja niwaambie tena neno gumu leo; huwezi kukuta popote historia ya mtu imeandikwa ambaye hakuchukua hatua yoyote ya kutenda, jambo liwe jema au baya!!**
- **Lakini hata inzi hapigwi kibao hadi pale anapochukua hatua ya kuja kutua juu ya chakula chetu!! Kwa hiyo kuishi ndani ya wokovu wakati unaogopa kuchukua hatua za imani juu ya Neno la Mungu ninalokufundisha kila siku ni kitendo ambacho kimekuchelewesha mno kuiona miujiza yako (Ni kitendo ambacho kinanyonga kila siku/kinakaba Baraka zako zisiwe halisi kwako.) na watendaji wa Neno watatoka nyuma na kukupita kila siku**.

***Note:*** **Kuja kanisani wapendwa ni sawa na mtu kupeleka gari lake gereji; huko utakuta mafundi ambao kazi yao ni kulifungua na baadaye kulifunga; mwenye gari akiwataka mafundi waone tatizo na halafu awazuie kuchukua hatua watamshangaa kwa nini amelipeleka gari lake huko!!! Ndiyo walivyo wateule wengi, wanakuja Kanisani, wanajiangalia katika kioo (Neno la Mungu) na kisha wanaondoka pasipo kuchukua hatua!! Kumbe wangejitosa kama Daudi au kama wale Wakoma wanne au kama Esta alivyojitosa na kusema liwalo na liwe, au kama Ruthu aliyejitosa au kama Ibarahimu alivyojitosa au kama mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu**

**alivyojitosa, au kama Zakayo alivyojitosa; ndoto zao nyingi sana zingeshakuwa dhahiri kuliko walivyo sasa**.

- Leo niwaambie kabisa wateule wenzangu, kama roho ya woga itaendelea kutawala maisha yetu kiasi cha kutuzuia/kutuhofisha kuchukua hatua za imani katika mambo ambayo Mungu Baba anasema nasi siku zote, tusitazamie kabisa kumwona Yesu na matendo yake ya ajabu katika maisha yetu na wala tusitazamie kuona historia mpya inaandikwa katika maisha yetu. ***Math. 14: 28 – 31.*** Tusiruhusu kabisa mashaka/hofu/woga wetu kuwa mkubwa kuliko imani tuliyonayo juu ya Yesu wetu aliyeshinda kabisa. ***Uf. 1: 17 -18.***

- Yesu anawaambia wanafunzi wake siku ya chakula cha mwisho kabla hajaenda kusulubiwa kwamba wakumbuke na wala wasisahau kwamba kitendo chake cha kujitoa kuteswa na kusulubiwa na kuuawa ndiyo siri ya wokovu wetu, anaukabili msalaba kwa ujasiri akijua baadaye kuna furaha kubwa na heshima ya hali ya juu atakayopewa na Baba yake – wakumbuke hili jambo katika maisha yao yote ya utumishi. ***Luk. 22: 14 – 20, Ebr. 12: 1- 3.***

- Mwanamke yeyote akiogopa utungu, hatakubali kuzaa mtoto wa pili, ukiona wengine wamezaa hadi **3 – 8**, walijitosa!!! Huwezi kulinganisha baadaye furaha yao na Yule aliyezaa kamoja tu kwa hofu ya kuogopa kufa akaacha - lazima tuchukue hatua, lazima tujitose sasa ili Bwana Yesu aonekane dhahiri katika maisha yetu ya wokovu. **Amina.**

***Na***
***Askofu Dr. L.M. Mwizarubi***
***July 2022.***